

# HALMASHAURI YA MANISPAA TEMEKE

*[Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa Temeke]*

Simu: +255 22-292832  
Fax: +255 22-2928137  
Barua pepe: temeke@temekemc.go.tz  
Tovuti: <http://www.temekemc.go.tz>



Ofisi ya Mkurugenzi  
92 Barabara ya Mandela/Taifa  
S.L.P: 46343,  
**15833** - DAR ES SALAAM,

**Kumb Na.** TMC/MD/E.5/1/13

**Tarehe:** 01/11/2021

## NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke alipokea kibali cha ajira mbadala kutoka kwa Katibu Mkuu Utumishi chenye Kumb.Na.**FA.170/374/01/"A"/68** cha tarehe **20 Oktoba, 2021** kwa ajili ya kuajiri **Katibu Mahsusi Daraja la III nafasi 1.**

Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi ya kazi iliyoainishwa katika tangazo hili, kama ifuatavyo:

### 1.1 KATIBU MAHSUSI DARAJA III (NAFASI 01) TGS B

#### **1.2 SIFA ZA MWOMBAJI**

- I. Awe na Elimu ya kidato cha IV au VI.
- II. Awe na cheti cha Astashada (**Technician Certificate – NTA Level 5**) cha masomo ya Uhazili kutoka katika Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti cha mafunzo ya kompyuta katika programu za Windows, Microsoft Office, Internet, E. mail na Publisher.
- III. Awe amefaulu somo la Hati Mkato la Kingereza na Kiswahili maneno 80 kwa dakika moja

## **KAZI NA MAJUKUMU**

- Kuchapa barua na nyaraka mbalimbali
- Kusaidia kutunza kumbukumbu za matukio, miadi, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba za kazi zilizopangwa kutekelezwa katika ofisi anayofanyia kazi na kumuarifu mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
- Kusaidia kuwapokea wageni na kuwasikiliza shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika kazi
- Kutekeleza kazi zote zitakakuwa amepangiwa na msimamizi wake wa kazi.

## **MASHARTI YA JUMLA**

- i. Awe Mtanzania mwenye umri wa kuanzia miaka 18 lakini asizidi umri wa miaka 45.
- ii. Awe na afya njema, mchapakazi na mwenye utayari wa kufanya kazi mahali popote Manispaa ya Temeke
- iii. Unatakiwa kuwa na namba ya utambulisho wa Uraia kutoka mamlaka ya vitambulisho vya Taifa NIDA.
- iv. Mwombaji awasilishe picha moja ya hivi karibuni (**Passport size**) iliyoandikwa jina nyuma
- v. Waombaji wawasilishe maelekezo binafsi yanayojitosheleza (**Detailed CV**) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini watatu (Referees) wa kuaminika.
- vi. Waombaji wote waambatanishe **nakala ya vyeti halisivya kidato cha IV na VI** kwa wale walifika kiwango hicho masomo na Taaluma (**Technician Certificate – NTA Level 5**), **Transcript ya cheti cha**

taaluma na **Cheti cha kuzaliwa**. Mwombaji atakayewasilisha “Result Slip”, “Statement of Result”, “Provisional Result” au Transcript bila nakala halisi ya cheti cha Taaluma maombi yake hayatakubaliwa.

- vii. Kwa waliosoma nje ya Nchi Elimu ya kidato cha nne na kidato cha sita wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA)
- viii. Maombi yasiyozingatia vigezo vilivyoainishwa hayatashughulikiwa
- ix. Barua ya Maombi indikwe kwa mkono na kusainiwa kisha yatumwe kwa njia posta kupitia anuani iliyotajwa hapo chini.
- x. Maombi yatapokelewa katika ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke katika kipindi cha siku 14 kuanzia tarehe ya tangazo hili na mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 14/11/2021

Maombi yote yatumwe kwa:-

Mkurugenzi,  
Halmashauri ya Manispaa ya Temeke,  
S. L. P 46343,  
**DAR ES SALAAM**

Tangazo hili linapatikana pia katika wavuti ya Manispaa ([www.temekemc.go.tz](http://www.temekemc.go.tz)) na wavuti wa Serikali ya Ajira katika Utumishi wa Umma([www.ajira.go.tz](http://www.ajira.go.tz)).

Imetolewa na

  
Elihuruma Mabelya  
**MKURUGENZI WA MANISPAA TEMEKE**  
MKURUGENZI WA MANISPAA  
TEMEKE